

KAZI YA LIKIZO KIDATO CHA PILI

Matumizi ya lugha

1. (a) **Badilisha sentensi ifuatayo iwe mazoea kwa kutumia kirejeshi “O”**
 Mtoto anayelia huchapwa
- (b) **Andika kinyume**
 Wavulana watatu wanaingia darasani kwa haraka.
- (c) **Andika sentensi tatu ambazo zaweza kuwa sahihisho la sentensi hii:-**
 Kule ndimo alipoingia
- (d) **Taja aina za vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo**
 Mama amewahi kupika jikoni
- (e) **Eleza maana ya misemo ifuatayo.**
- (i) Giza la ukata...
- (ii) Meza mate machungu
- (f) **Unda vitenzi kutokana na;**
- (i) Mkufunzi
- (ii) Maeneo
- (g) **Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, taja aina za sentensi za kiswahili**
- (i) **Eleza maana mbili za sentensi ;**
 Mama alimlimia mwanawe shamba
- (j) **Akifisha sentensi ifuatayo:**
 ah huu ndio upuuzi aliotuitia mmoja wao akaropoka.
- (k) **Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha namna mfanano**
- (l) **Andika sentensi ifuatayo katika msembo halisi :**
 Mshtakiwa alidai kwamba alikuwa ameonewa kwa kuwa hakuwa ameshiriki ulevi kutoka mwaka uliokuwa umetangulia.
- (m) **Pambanua viungo vya kisarufi katika kitenzi kifuatacho**
 Tuliwalimia
- (n) **Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:**
 Mizizi ya mibaruti hii iliwaponya watu ambao walikuwa na shida kama hii yenu (**kanusha kwa umoja**)
- (o) **Tunga sentensi ukitumia neno “Vile” kama:**
- (i) Kiwakilishi
- (ii) Kivumishi
- (iii) Kielezi
- (p) **Bainisha matumizi ya viambishi “ku” na “Ji” katika sentensi zifuatazo:-**
- (i) Mwanafunzi hukusoma kwa bidii
- (ii) Atakupiga
- (iii) Amejukata
- (iv) Mchezujaji huyu ni hodari
- (q) **Andika sentensi ifuatayo kwa ukubwa huku ukikanusha**
 Kijibwa changu ni kikali sana
2. (a) **Jaza mapengo:-**
- | | |
|--------------------------------|-------------------|
| Kutenda | Kutendesha |
| (i) Chota | |
| (ii) Lewa | |
| (b) Taja sauti moja ya; | |
| (i) King’ong’o | |

- (ii) Kiyeyusho
- (c) **Tumia neno “shujaa” katika sentensi kama:**
- (i) Kivumishi
 - (ii) Kielezi...
- (d) **Tambua vitenzi katika sentensi hii kwa kuvipigia mistari:**
Sisi tulikwisha kutambua alikuwa na nia mbaya. Yeye ndiye mwizi
- (e) **Andika wingi wa sentensi hii katika hali ya ukubwa:**
Kichinjio hiki kilikarabatiwa kwa pesa nyingi
- (f) **Eleza maana zinazojitokeza katika vifungu vifuatavyo:**
- (i) Jambazi kutoka dukani liliiba.
 - (ii) Liliiba jambazi kutoka dukani.
 - (iii) Kutoka dukani jambazi liliiba.
 - (iv) Jambazi liliiba kutoka dukani.
- (g) **Jaza neno ambalo ni kinyume cha lile lililopigwa mstari katika sentensi:**
- (i) Vile vitu ulivyovichanganya itakubidi uviangalie
 - (ii) Bomba hili limeziba mwite fundi
- (i) **Eleza matumizi mawili ya “ka” na utunge sentensi kwa kila mojawapo**
- (j) **Yakinisha sentensi hii:**
Sijafahamu kwa nini hawamkaribisha mpwa wao.

